TANGAZO LA SERIKALI NA. 336 la tarehe 5/5/2023

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 157)*

KANUNI ZA USAFIRI MAJINI ZA UCHUNGUZI WA AFYA ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTEUZI, SIFA NA ENEO LA DAKTARI KUFANYIA KAZI

4. Uteuzi wa daktari.
5. Kusitisha au kufuta uteuzi wa daktari.
6. Sehemu au eneo kwa ajili ya uchunguzi wa afya.
7. Uhamisho wa eneo.

SEHEMU YA TATU
CHETI CHA UTIMAMU WA AFYA

8. Ajira kwa baharia.
9. Sifa ya kupata cheti cha utimamu wa afya.
10. Kiwango cha utimamu wa afya.
11. Uhalali wa cheti.
12. Umiliki wa cheti cha utimamu wa afya.
13. Utambuzi wa cheti cha utimamu wa afya kilichotolewa na nchi nyingine.
14. Kusitisha au kufuta cheti cha utimamu wa afya.

15. Cheti cha ustadi na cheti cha umahiri.

SEHEMU YA NNE
MAKOSA NA ADHABU

16. Makosa chini ya Kanuni hizi.
17. Adhabu ya jumla.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

18. Mfumo wa viwango vya ubora.
19. Taarifa za afya ya baharia au nahodha.
20. Rejesta.
21. Ushughulikiaji wa malalamiko.
22. Kufutwa kwa Kanuni na masharti yanayoendelea kutumika.

MAJEDWALI

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 157)*

KANUNI ZA USAFIRI MAJINI ZA UCHUNGUZI WA AFYA ZA MWAKA 2023

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Usafiri Majini za Uchunguzi wa Afya za mwaka 2023.

Matumizi

2.-(1) Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo, Kanuni hizi zitatumika katika kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo, Utoaji Vyeti na Ufanyaji Kazi Melini kwa Mabaharia, 1978 na Mkataba wa Kimataifa wa Ajira za Mabaharia, 2006 kama ilivyorekebishwa.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kanuni ndogo ya (1), Kanuni hizi zitatumika kwa-

TS. Na. 243 la 2016

(a) baharia au nahodha mwenye cheti halali cha matibabu na mwenye cheti cha Tanzania kilichotolewa chini ya Kanuni za Usafiri Majini za Mafunzo, Utoaji Vyeti na Idadi na Sifa za Wafanyakazi Melini bila kujali ukubwa wa meli anayofanya kazi au anayokusudia kufanya kazi; na
(b) baharia au nahodha wa meli zinazosafiri baharini ambazo si meli za Tanzania, zinapokuwa katika bandari ya Tanzania.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2), Kanuni hizi hazitatumika kwa:

(a) vyombo vya starehe;
(b) vyombo vya uvuvi;
(c) meli za kivita au usaidizi wa jeshi la wanamaji;
(d) vyombo vya majini vinavyomilikiwa na kuendeshwa na idara au wakala wa Serikali kwa madhumuni yasiyo ya kibiashara; na

(e) mitambo iliyosimikwa baharini wakati inapokuwa katika maeneo yake ya kazi.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"baharia" inajumuisha kila mtu isipokuwa nahodha wa meli, rubani au mwanagenzi aliyeingia mkataba na ambaye amesajiliwa, ameajiriwa au anafanya kazi katika nafasi yoyote ndani ya meli;

Sura ya 152

"daktari" ina maana iliyoainishwa chini ya Sheria ya Matabibu, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi;

"mmiliki" kuhusiana na meli, au "mmiliki wa meli" maana yake, kwa meli iliyosajiliwa, ni mmiliki aliyesajiliwa na inajumuisha mkodishwaji mwenye majukumu yote na mmiliki mwendeshaji au wakala mwendeshaji;

"Notisi" maana yake ni Notisi ya Usafiri Majini iliyotolewa na Msajili;

"cheti cha utimamu wa afya" maana yake ni cheti cha afya cha baharia kilichotolewa chini ya Kanuni hizi;

"daktari mwamuzi" maana yake ni mmoja wa madaktari aliyeteuliwa na Msajili kufanya mapitio ya uchunguzi wa mabaharia au nahodha kwa mujibu wa kanuni ya 21 ya Kanuni hizi;

"meli" maana yake ni chombo kinachoelea ambacho kinajiendesha na chenye uwezo wa kubeba abiria au mizigo na inajumuisha kila aina ya chombo kinachotumika katika usafari majini;

"Mkataba wa STCW" maana yake ni Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo, Utoaji Vyeti na Ufanyaji Kazi Melini kwa Mabahariawa mwaka 1978, kama ulivyofanyiwa marekebisho;

Sura ya 415

"Msajili" maana yake ni Msajili aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"nahodha" maana yake ni mtu, isipokuwa rubani,

mwenye amri au jukumu la usimamizi wa meli, ndege ya baharini au chombo kingine kikiwa juu au karibu na maji;

Sura ya 165

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Usafiri Majini;

Sura ya 415

"Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lilioanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania.

## SEHEMU YA PILI
## UTEUZI, SIFA NA ENEO LA DAKTARI KUFANYIA KAZI

Uteuzi wa daktari

4.-(1) Shirika linaweza kuteua daktari kwa madhumuni ya kufanya uchunguzi kwa mabaharia au nahodha kwa ajili ya kubaini utimamu wa afya zao.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), daktari aliyeteuliwa anapaswa kuwa na uzoefu wa kazi ya utabibu kwa muda usiopungua miaka mitano.

(3) Daktari anayetaka kuteuliwa atapaswa kuwasilisha kwa Shirika nyaraka zifuatazo:

(a) vyeti husika vya taaluma; na
(b) cheti cha usajili kinachotolewa na chombo husika cha ithibati ya matibabu.

(4) Katika kuhakiki uhalisi na uhalali wa nyaraka zilizoambatishwa katika maombi, Shirika linaweza kumtaka daktari kutoa taarifa za nyongeza kadiri litakavyoona inafaa.

(5) Shirika litaingia katika makubaliano ya kimaandishi na daktari aliyeteuliwa kuhusiana na usimamizi na utoaji wa huduma ya uchunguzi wa afya kwa mabaharia.

Kusitisha au kufuta uteuzi wa daktari

5.-(1) Uteuzi wa daktari unaweza kusitishwa au kufutwa na Shirika kwa maandishi-

(a) kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa katika uchunguzi au taarifa ya ukaguzi na mamlaka husika;
(b) endapo daktari amehama sehemu au eneo analofanyia kazi yake ya kitabibu kwenda sehemu au eneo lingine bila kutoa taarifa kwa Shirika;
(c) pale ambapo, kwa maoni ya Shirika, mazingira

yanalazimu kusitisha au kufuta uteuzi;

(d) baada ya usajili wa daktari kubatilishwa na chombo husika cha ithibati ya madaktari. ;

(e) endapo daktari atashindwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi.

(2) Endapo Shirika litafanya uamuzi wa kusitisha au kufuta uteuzi wa daktari, litatoa notisi ya maandishi ya siku thelathini.

(3) Ikiwa ni kusitisha uteuzi, Shirika litaainisha muda wa kusitishwa au masharti ambayo yakitimizwa yatapelekea kuondoa sitisho.

Sehemu au eneo kwa ajili ya uchunguzi wa afya

6.-(1) Uchunguzi wa afya ya mabaharia au nahodha utafanyika katika sehemu au eneo ambalo limesajiliwa na mamlaka husika.

(2) Sehemu au eneo husika litakua na miundombinu na vifaa vinavyohitajika katika kufanya uchunguzi wa utimamu wa afya na kufikika kwa urahisi.

(3) Shirika litafanya ukaguzi wa eneo na vifaa ili kuthibitisha kama vinafaa katika kufanya uchunguzi wa utimamu wa afya.

Uhamisho wa eneo

7.-(1) Daktari anayekusudia kuhamisha huduma zake kwenda eneo lingine atalitaarifu Shirika kwa maandishi angalau siku tano kabla ya mabadiliko hayo.

(2) Baada ya kupokea taarifa katika kanuni ndogo ya (1), Shirika litafanya uhakiki wa eneo husika ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa.

## SEHEMU YA TATU
## CHETI CHA UTIMAMU WA AFYA

Ajira kwa baharia

8.-(1) Mmiliki wa meli au nahodha atamwajiri baharia mwenye cheti halali cha utimamu wa afya kinachofaa kwa eneo ambalo meli itafanya kazi au kwa kazi ambayo baharia ataajiriwa kufanya kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Baharia atachukuliwa kuwa mwenye utimamu wa afya endapo-

(a) ana cheti halali cha utimamu wa afya;

(b) hakuna ushahidi kwamba hali yake ya kiafya imebadilika tangu uchunguzi wa awali wa kiafya kiasi ambacho kingeweza kumfanya ashindwe kutekeleza majukumu yake kama inavyotakiwa; au

(c) imethibitishwa kuwa ana cheti cha utimamu wa afya kilichoisha muda wake karibuni na inawezekana kwa baharia kuchunguzwa na kupata cheti cha utimamu wa afya katika bandari inayofuata.

(3) Endapo cheti cha utimamu wa afya cha baharia kitaisha muda wake wakati wa safari, mmiliki wa meli au nahodha anaweza kuendelea kumwajiri baharia-

(a) kwa muda usiozidi miezi mitatu kuanzia tarehe ya kuisha muda kwa cheti cha utimamu wa afya, au

(b) mpaka kwenye bandari nyingine ambayo baharia anaweza kuchunguzwa na kupata cheti cha utimamu wa afya, mradi ana cheti cha utimamu wa afya ambacho muda wake umekwisha karibuni;

chochote kitakachotangulia.

(4) Msajili anaweza kumruhusu baharia mwenye cheti cha utimamu wa afya kilichoisha muda wake ndani ya mwezi kabla ya tarehe ambayo baharia alijiunga na meli zinazoguswa na Kanuni hizi, kuajiriwa licha ya kuisha muda wa cheti, hadi bandari nyingine ambapo baharia atapata cheti cha utimamu wa afya kwa mujibu wa Kanuni hizi:

Isipokuwa, muda wa ruhusa hiyo hautazidi miezi mitatu.

(5) Mmiliki wa meli au nahodha atakayekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Dola za Marekani elfu mbili au kiwango sawa na hicho kwa shilingi za Tanzania.

Sifa za kupata cheti cha utimamu wa afya

9.-(1) Baharia au nahodha anayekusudia kupata cheti cha utimamu wa afya, atapaswa-

(a) kuwa na umri wa angalau miaka kumi na nane;
(b) kutoa uthibitisho wa kuridhisha unaomtambulisha baharia; na
(c) kufanyiwa uchunguzi wa afya ili kuhakiki utimamu wake, kwa kuzingatia viwango vya kitabibu kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 10.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), baharia mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nane lakini mwenye zaidi ya miaka kumi na sita anaweza kupata cheti cha utimamu wa afya kwa madhumuni ya kupata mafunzo melini.

(3) Cheti cha utimamu wa afya-
(a) kitakuwa katika lugha ya Kiingereza na katika muundo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza; na
(b) kitatoa taarifa endapo mwombaji anafaa au hafai kufanya kazi ya ubaharia aliyoajiriwa kuifanya.

(4) Endapo uoni wa rangi unatiliwa shaka, daktari anaweza, kwa kuzingatia majukumu atakayoyafanya baharia au nahodha akiwa baharini, kuendelea kufanya kipimo cha uthibitisho wa uoni wa rangi-
(a) kwa kutumia kituo kilichoteuliwa na Shirika; na
(b) kwa mujibu wa viwango vya chini vya uoni kwa baharia au nahodha.

Kiwango cha utimamu wa afya

10.-(1) Uchunguzi wa afya ya baharia au nahodha kwa ajili ya utoaji wa cheti cha utimamu wa afya utazingatia viwango vya-
(a) kuona na uoni; na
(b) usikiaji.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), viwango vitakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Kipimo cha kuona na uoni wa rangi kitakachofanyika kitakuwa halali kwa kipindi kisichozidi miaka sita.

(4) Shirika linaweza kuteua mahali kama kituo

cha rufaa kwa madhumuni ya kutathmini uwezo wa uoni wa rangi ili kumpa daktari taarifa muhimu kwa ajili kutoa cheti cha utimamu wa afya.

Uhalali wa cheti

11. Muda wa uhalali wa cheti cha utimamu wa afya utakuwa kama ifuatavyo:

(a) kwa baharia ambaye hajatimiza umri wa miaka kumi na nane, muda usiozidi mwaka mmoja; na

(b) kwa baharia aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane, muda usiozidi miaka miwili.

Umiliki wa cheti cha utimamu wa afya

12. Baharia au nahodha aliyepewa cheti cha utimamu wa afya-

(a) atahakikisha kwamba cheti halisi kipo katika umiliki wake muda wote atakapokuwa kwenye meli kwa kipindi cha ajira yake; na

(b) ataonesha cheti hicho pale ambapo atahitajika kufanya hivyo na mkaguzi au mchunguzi.

Utambuzi wa cheti cha utimamu wa afya kilichotolewa na nchi nyingine

13. Cheti cha utimamu wa afya kilichotolewa na mamlaka ya serikali ya nchi nyingine katika kutekeleza mashati ya Mkataba wa STCW au nchi iliyoainishwa katika Notisi ya Usafiri Majini kitakuwa sawa na cheti cha utimamu wa afya kilichotolewa chini ya Kanuni hizi.

Kusitisha au kufuta cheti cha utimamu wa afya

14.-(1) Shirika linaweza-

(a) kusitisha cheti mpaka pale baharia atakapofanya uchunguzi mwingine wa afya na kuidhinishwa;

(b) kusitisha cheti kwa muda ambao baharia hataweza kusafiri baharini kama itakavyopendekezwa na daktari au;

(c) kufuta cheti endapo daktari atapendekeza kwamba baharia hataweza kamwe kusafiri baharini.

(2) Shirika litasitisha au kufuta cheti pale endapo litakuwa na sababu za msingi kuamini kwamba-

(a) kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kiafya ambayo yanaathiri utimamu wa afya ya baharia

au nahodha wakati wa uhalali wa cheti chake; na,

(b) cheti cha utimamu wa afya kilitolewa kwa baharia au nahodha kinyume na matakwa ya Kanuni hizi.

(3) Endapo Shirika limesitisha au kufuta cheti kilichotolewa chini ya Kanuni hizi, litamjulisha baharia au nahodha kuhusu uamuzi huo kwa maandishi.

(4) Shirika litamwelekeza baharia au nahodha ambaye cheti chake kimesitishwa au kufutwa chini ya kanuni ndogo ya (1) kusalimisha cheti hicho kwa Shirika ndani ya siku saba.

(5) Ikiwa cheti kimesitishwa, Shirika litaainisha muda au masharti ambayo yakitekelezwa yatasababisha sitisho kuondolewa.

Cheti cha ustadi na cheti cha umahiri

15. Cheti cha utimamu wa afya kilichotolewa chini ya Kanuni hizi kitakubalika kama uthibitisho wa utimamu wa afya ya baharia au nahodha anayeomba kupewa au uthibitisho wa cheti cha ustadi au umahiri.

## SEHEMU YA NNE
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa chini ya Kanuni hizi

16.-(1) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi kwa:

(a) kumwajiri baharia asiyekuwa na cheti hai cha utimamu wa afya kinachofaa kwa eneo atakalofanya kazi katika meli;

(b) kutoa taarifa isiyo sahihi au nyaraka zisizo sahihi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua thamani ya shilingi za Tanzania sawa na Dola za Marekani elfu tano au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote.

(2) Daktari atakayetoa cheti cha utimamu wa afya-

(a) bila kuteuliwa na Shirika; au

(b) wakati uteuzi wake wa kutoa huduma ya uchunguzi wa afya kwa mabaharia umesitishwa

au umefutwa na Shirika,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua thamani ya shilingi za Tanzania sawa na Dola za Marekani elfu tano au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote.

(3) Baharia ambaye atashindwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua thamani ya shilingi za Tanzania sawa na Dola za Marekani elfu mbili.

Adhabu ya jumla

17. Endapo mtu atatenda kosa ambalo adhabu yake haijatamkwa katika Kanuni hizi, akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika Sheria.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Mfumo wa viwango vya ubora

18.-(1) Shirika litasimamia shughuli za uthibitisho wa utimamu wa afya kupitia Mfumo wa Viwango vya Ubora.

(2) Mfumo wa Viwango vya Ubora utaweka taratibu na viwango vya chini vya-

(a) utoaji wa vyeti vya afya;
(b) uteuzi wa daktari; na
(c) mapitio ya uamuzi wa Shirika.

Taarifa za afya ya baharia au nahodha

19.-(1) Nakala za vyeti vya afya vya mabaharia au nahodha zitawekwa katika majalada katika eneo au kituo ambapo cheti kimetolewa na kitawekwa alama ya usiri.

(2) Taarifa za uchunguzi wa afya-

(a) zitatunzwa kwa siri;
(b) zitatumika kwa ajili ya kutathmini utimamu wa baharia au nahodha katika kazi na kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya;
(c) zitatolewa kwa mtu aliyeidhinishwa pekee; na
(d) hazitatumika kwa madhumuni mengine isipokuwa kuwezesha matibabu ya baharia au nahodha.

(3) Taarifa za afya hazitafichuliwa kwa mtu

mwingine yeyote bila idhini ya maandishi ya baharia au nahodha.

Rejesta

20.-(1)- Shirika-

(a) litahifadhi na kutunza Rejesta itakayokuwa na taarifa kuhusiana na uchunguzi wa afya kwa madhumuni ya Kanuni hizi; na

(b) litawezesha upatikananji wa Rejesta kwa maombi ya nchi yoyote, kampuni au baharia.

(2) Taarifa katika Rejesta iliyorejewa katika kanuni ndogo ya (1) zitajumuisha-

(a) taarifa za madaktari walioteuliwa chini ya Kanuni hizi; na

(b) majina ya nchi ambazo vyeti vyao vya afya vinatambuliwa na Shirika.

Ushughulikiaji wa malalamiko
TS. Na.
338 la 2018

21.-(1) Baharia au nahodha ambaye hajaridhika na uamuzi chini ya kanuni ya 14 anaweza kuwasilisha kwa Shirika maombi ya mapitio ya uchunguzi na daktari mwamuzi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), maombi ya mapitio ya uchunguzi yatawasilishwa kwa Shirika ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ambayo uamuzi ulitolewa.

(3) Baada ya kupokea maombi ya mapitio ya uchunguzi, Shirika litashughulikia maombi hayo na kuwasilisha uamuzi wake kwa mwombaji ndani ya siku kumi na nne.

Kufutwa kwa Kanuni na masharti yanayoendelea kutumika
TS. Na.
244 la 2016

22.-(1) Kanuni za Usafirishaji Majini (Uchunguzi wa Afya) zinafutwa.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), cheti cha utimamu wa afya kilichotolewa kwa baharia au nahodha chini ya Kanuni za Usafirishaji Majini (Uchunguzi wa Afya) kitaendelea kutumika hadi tarehe ya mwisho ya kutumika kama ilivyoainishwa kwenye cheti.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI**

JEDWALI LA KWANZA

_________________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9(3))*

CHETI CHA UTIMAMU WA AFYA

Cheti hiki kimetolewa kwa kuzingatia:

(a) Kanuni za Usafiri Majini (Mafunzo, Utoaji Vyeti na Idadi na Sifa za Wafanyakazi Melini), TS. Na. 243/ 2016;
(b) Kanuni za Usafiri Majini (Uchunguzi wa Afya), 2023;
(c) Kanuni za Usafiri Majini (Ajira za Mabaharia), TS. Na. 228/2022;
(d) Kanuni ya I/9 ya Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo, Utoaji Vyeti na Ufanyaji Kazi Melini kwa Mabaharia 1978, kama ilivyorekebishwa (STCW);
(e) Kanuni ya 1.2 ya Mkataba wa Kimataifa wa Ajira za Mabaharia (MLC,2006).

Taarifa za Baharia au Nahodha:

Jina la Ukoo……………………. Jina la Kwanza…………………………Jina la Kati………………………

Tarehe ya Kuzaliwa (Siku/Mwezi/Mwaka …./…./….Jinsia: Me ☐ Ke ☐

Makazi ya Kudumu: …………………………………………………………………………………

Aina ya Kitambulisho:……..........................…………….. Na.: ……………. Utaifa: …………………………........

Idara: Injini ☐ taha ☐ shi ☐ inezo (Ainisha): ……………....................

Nimemkagua mwombaji aliyetajwa hapo juu kulingana na viwango vya utimamu wa afya vya baharia na mahitaji ya uthibitisho yaliyowekwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni I/9 ya Mkataba wa STCW wa 1978 kama ulivyorekebishwa na kanuni ya 1.2 ya Mkataba wa Ajira za Mabaharia wa 2006 kama ilivyorekebishwa.

Kwa msingi wa tamko binafsi la mwombaji, uchunguzi wangu wa afya na matokeo ya vipimo vya afya vilivyoandikwa kwenye fomu ya uchunguzi wa matibabu, ninathibitisha kuwa mwombaji kwa mujibu wa maombi aliyoleta:

Anafaa: ☐

Hafai: ☐

Kwa masharti:.......................................................................................................

Maelezo ya Masharti...........................................................................................

Tiba inayopendekezwa:........................................................................................

Nathibitisha yafuatayo: (Weka tiki inapostahili: Uoni:

Uwezo wa kuona: Ndio ☐ ensi za mawasiliano ☐

Hapana ☐

Miwani ☐ Msaada wa uono ☐

Maoni ya rangi: Ndio ☐ Hapana ☐

Tarehe ya mwisho ya kipimo cha kiwango cha uonaji:
……………………Mwezi…………….., 20………

(Zingatia: kipimo cha uonaji rangi hakihitajiki kwa vyeti vya kitaifa vya uhandisi)

Usikivu: Ndio ☐

Hapana ☐

Majukumu ya kuangalia usalama (Idara ya Sitaha pekee):

Ndio ☐

Hapana ☐

Uwezo wa kusikia:

Ndio ☐

Hapana ☐

Wakuridhisha ☐

Usaidizi wa kusikia:

Ndio ☐

Hapana ☐

Uwezo wa kuangalia usalama:

Ndio ☐

Hapana ☐

Majukumu ya kuridhisha:

………………………………………………………………………………

Tarehe ya uchunguzi: …..……/..………/……………… Sehemu ya

uchunguzi………………………………

Tarehe ya ukomo wa cheti: ………/………../……………

Jina la Daktari:

……………………………………………………………………….................

Sahihi ya Daktari: …………………………………...

Muhuri wa moto: ..........................................................

Ninakiri kwamba nimeshauriwa kuhusu maudhui ya taarifa ya uchunguzi wa afya na haki yangu ya kutafuta mapitio ya maudhui ya cheti hiki. Katika kipindi cha mabadiliko ya hali yangu ya afya, ninakubali uhalali wa cheti kupitiwa upya na Daktari.

Sahihi ya mwombaji: ………………………… (imesainiwa mbele ya Daktari)

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA**

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 21(1))*

TSC-DMSE-SMERRF

FOMU YA MAOMBI YA MAPITIO YA UCHUNGUZI WA AFYA KWA BAHARIA

**A.** TAARIFA ZA MUOMBAJI

Namba ya Hati ya Kusafiria Na. / CDC Na. (Kitabu cha Kushuka Melini)
Tarehe ya kuzaliwa
.......................................................................................................................
TR...........MZ...........MK.................

Jina kamili Bw./ Bibi./Bi.:
..............................................................................................................................

Mahali pa kuzaliwa:

Wilaya:.........................................Mkoa:...........................Uraia:..........................

Anuani ya kudumu (kwa mawasiliano)

Mtaa:....................................... Na. Ya Mkazi:.......................... S.L.P…………………
Mji/Jiji………………………..

Anuani ya kupokelea (kama ni tofauti)

………………………………………………………………………………………………
………………………………..

Namba za Simu:
…………………………………………………….

Barua pepe: …………………………………………………….

**B.** UCHUNGUZI WA KAZI ATAKAYOFANYA: (weka tiki inapostahili)

Sitaha ☐ Injini ☐ Upishi ☐

Mengineyo (ainisha):
………………………………………………………………………………………………
………

Tarehe ulipofanyika uchunguzi wa afya unaombewa marejeo:
………………………………………………………………………………………………
………………………………..

SAHIHI YA MWOMBAJI NA PICHA

Tafadhali tumia kalamu ya wino mweusi

Sahihi ☐ Picha ☐

**C.** SABABU ZA UCHUNGUZI MWINGINE

Tafadhali onesha hapa chini sababu za marejeo ya uchunguzi, ambatisha nyaraka zinazohusika.
Sababu:………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

**D.** TAMKO

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa katika ombi hili la uchunguzi mwingine ni za kweli na zimekamilika. Nathibitisha kuwa nyaraka nilizowasilisha ni halisi, na Ninaelewa kuwa ombi langu la kufanyiwa uchunguzi mwingine halihitaji malipo kwa kila matokeo au uamuzi unaopitiwa.

Sahihi ya mwombaji: ………………………………………………

Tarehe: ………………………………............................................

Kumb.: Majibu ya uchunguzi mwingine yatatolewa na mamlaka ndani ya siku kumi na nne tangu kutumwa kwa maombi.

**E.** MAONI YA DAKTARI MWAMUZI

Maoni:
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

……………………………………………….. …………………………………….
Jina Wadhifa
………..……………………… ……………………
Sahihi Tarehe

**F.** KWA MATUMIZI YA OFISI

SEHEMU A: UTHIBITISHO WA AFISA

Maoni:
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

……………………… …………………………
Sahihi Tarehe

SEHEMU B: MAPENDEKEZO YA MENEJA WA MABAHARIA

Maombi haya yamepitishwa ☐ hayajapitishwa ☐

Maoni:
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

……………………… …………………………
Sahihi Tarehe

SEHEMU C: KIBALI CHA MSAJILI

Maombi haya yameidhinishwa ☐ hayajaidhinishwa ☐

Maoni:
…………………..........................……………………………………….................
…………………………………………………………………………………..

Dodoma
20 April, 2023

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*